

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA
(Barua zote zitumwekwaMkurugenziMtendajiWilaya)**



Simu. Na. 220 2325/2261
Fax Na. 220 2472
E-mail: ded@lindidc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
306 Barabara ya Masasi,
S. L. P. 328,
65183 MTAMA-LINDI

Unapojibutafadhalitaja:-

Kumb. Na. *MDC/M.13/28/121*

19/04/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtama anapenda kuwatangazia watazania wote wenye sifa za nafasi za ajira za kudumu za Mtendaji wa Kijiji Daraja la III nafasi moja (1), Mwandishi Mwendesha Ofisi Daraja la III nafasi mbili (2), na Dereva Daraja la II nafasi mbili (2). Hii ni baada ya kupokea kibali cha ajira chenye Kumb.Na.FA.97/228/01"TEMP"/06 cha tarehe 06 Aprili, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliyotoa idhini ya kutekeleza lkama na Bajeti kwa ajira mpya katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mchanganuo wa nafasi za ajira ni kama ifuatavyo:-

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI MOJA (1)

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada /Cheti katika ngazi ya NTA leval 5 katika moja ya fani zifuatazo:Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI III

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na malizao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Kuratibu na Kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.

- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika kijiji.
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za kijiji,

MSHAHARA

mshahara ni TGS B Kwa kuzingatia waraka wa Serikali

2. MWANDISHI MWEENDESHA OFISI DARAJA LA III-NAFASI MBILI (2)

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amehitimu Elimu ya kidato cha IV na kuhudhuria mafunzo ya ngazi ya cheti/Astahada ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Awe amefaulu somo la Hati mkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo Kompyuta kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za **Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.**

KAZI NA MAJUKUMU YA MWANDISHI MWEENDESHA OFISI DARAJA LA III

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaidi shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake, na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitaji katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizihao.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa waliokatika sehemu alipo, au kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wakazi.

MSHAHARA

mshahara ni TGSB Kwa kuzingatia waraka wa Serikali

3.DEREVA DARAJA LA III-NAFASI MBILI (2)

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe mhitimu wa kidato nne (IV)
- Awe na leseni daraja "E" au "C-1" ya uendeshaji wa magari mbye amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewana Chuo cha Mafunzo Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi wa magari daraja la II itakua ni sifa ya ziada.

MSHAHARA

mshahara ni TGSB Kwa kuzingatia waraka wa Serikali

MASHARTI YA KAZI/WAOMBAJI KWA UJUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wasiozidi umri wa miaka 45.
- ii. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji ambaoni Watumishi wa Umma na wana sifa za kuingilia wapitishe barua zao za maombi kwa waajiri kuthibitisha kuridhia.
- iv. Nafasi ya Kazi inayoombwa iandikwe katika kichwa cha habari cha barua.
- v. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi **yanayojitosheleza (a detailed C.V)** yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya **wadhamini (referees) watatu** wakuaminika pamoja na namba zao za simu.
- vi. Maombi yote ya ambatane na nakala za vyeti vya taaluma na mafunzo kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali:
 - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV au VI.
 - Cheti cha mafunzo (professional).
 - Cheti cha kuzaliwa.
 - Picha Moja "Passport Size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- vii. "Testimonials", " Provisional results", "Statement of results ", hati matokeo za kidato cha IV na VI(form IV AND form VI results slips) **HAVITAKUBALIWA.**
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi zitapelekea wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Mwisho wa kupoke abarua za maombi ni tarehe **04/05/2023 saa 9:30** alasiri.
- x. Nakala ya Kitambulisho cha Taifa(NIDA) au Namba ya kitambulisho cha Taifa

Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kishwahili au Kiingereza na yatumwe kwa njia ya posta au moja kwa moja katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtama.

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 328,
MTAMA**

Limetolewa na;



George E. Mbilinyi
**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MTAMA**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MTAMA**